

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA AROBAINI NA NANE**

**11 JUNI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA NANE – TAREHE 11 JUNI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (*Monetary Policy Statement*) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**569. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya vya Chawi na Mnima zitatolewa.

**570. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Kamati za Watu Wenye Ulemavu zilizoanzishwa katika ngazi za Mikoa na Wilaya zinafanya kazi.

**571. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kuzitambua, kuzitengea Bajeti na kuziboresha Barabara za Vijiji vyenye uzalishaji mkubwa ili zipitike msimu wote.

**572. MHESHIMIWA SHEILA EDWARD LUKUBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mabweni kwa Wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita katika Shule ya Sekondari Nanenane.

**WIZARA YA UJENZI:**

**573. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Idweli hadi Ngumbulu - Rungwe yenye Km 26 itajengwa ili ipitike mwaka mzima.

**574. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENKA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Wananchi wanaoishi pembezoni mwa Barabara ya Ifakara - Mlimba wenye alama ya Kijani watalipwa fidia.

**575. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya lami itakayounganisha Wilaya tatu za Ulyankulu, Urambo na Sikonge.

**WIZARA YA KILIMO:**

**576. MHESHIMIWA DKT. NEEMA PETER MAJULE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Skimu za Umwagiliaji katika Mkoa wa Dodoma wenye tatizo la ukame.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**577. MHESHIMIWA EDWARD KISAU OLELEKAITA (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ukarabati wa Majosho Vijiji vya Ndotoi, Enguserosidan na Laiser katika Kata ya Laiser - Kiteto.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

##### **SAA 10:00 ALASIRI**

##### **WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA**  
**11 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD**  
**KATIBU WA BUNGE**